

**Scales representing the imbalance between insulin and sugar in the body for those with diabetes in Kenya. Colour lithograph by Ministry of Health, ca. 2000.**

**Publication/Creation**

Kenya : Wizara Ya Afya, [2000?]

**Persistent URL**

<https://wellcomecollection.org/works/k9q2vbkh>

**License and attribution**

Conditions of use: it is possible this item is protected by copyright and/or related rights. You are free to use this item in any way that is permitted by the copyright and related rights legislation that applies to your use. For other uses you need to obtain permission from the rights-holder(s).



Wellcome Collection  
183 Euston Road  
London NW1 2BE UK  
T +44 (0)20 7611 8722  
E [library@wellcomecollection.org](mailto:library@wellcomecollection.org)  
<https://wellcomecollection.org>



# UGONJWA WA KISUKARI NI NINI?

**Kisukari** ni hali ambayo mwili hukosa kutengeneza “insulini” inayotosha na hivyo kusababisha viwango vya juu vya sukari katika damu. (“Insulini” na kemikali itokayo kwenye kongosho inayorekebisha kiwango cha sukari kwenye damu).

Sukari hutumika mwilini kutupa nguvu. “Insulini” nayo husaidia sukari kufika kwenye sehemu za mwili kutupatia nguvu. Watu wasiokuwa na ugonjwa wa kisukari, kuna usawa kati ya sukari na “Insulini”.



Katika ugonjwa wa kisukari hakuna usawa kabisa baina ya “Insulini” na sukari kwa sababu mwili hautengenezi “insulini” ya kutosha. Hii ina maana kuwa mtu aliye na ugonjwa wa kisukari ana viwango vya juu vya sukari katika damu. Hali hii isipodhibitiwa inaweza kusababisha madhara mengi.

## Kuna aina mbili kuu za ugonjwa wa kisukari:

| AINA YA KWANZA   | AINA YA PILI   |
|--|--|
| Mwili hautengenezi “Insulini” yoyote                             | Mwili hautengenezi insulini ya kutosha au “insulini” haifanyi kazi inavyostahili   |
| Lazima mtu ajidunge sindano ya insulin. Mtu atahitaji “insulini” | Hutibiwa kwa chakula bora, mazoezi na tembe za kumeza. Mara nyingine “Insulini” hutumiwa kudhibiti aina hii ya ugonjwa wa kisukari |
| Kwa kawaida hutokea kwa watoto na vijana                         | Kwa kawaida, aina hii ya ugonjwa wa kisukari hutokea kwa watu wazima   |



Kituo cha udhabiti na habari za ugonjwa wa kisukari nchini Kenya

Kwa maelezo zaidi kuhusu ugonjwa wa Kisukari tembelea kituo cha afya kilichoko karibu nawe au kituo cha udhabiti na habari za ugonjwa wa kisukari nchini Kenya.

Nambari ya simu: 2718010/2733794



TAASISI YA UGONJWA WA KISUKARI DUNIANI